**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025]*

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
**DODOMA**

**April, 2026**

# YALIYOMO

*Ukurasa*

**YALIYOMO** .......... i
**ORODHA YA MAJENDWALI** .......... ii
**SEHEMU YA KWANZA** .......... 1
**1.0 MAELEZO YA JUMLA** .......... 1
1.1 Utangulizi .......... 1
1.2 Msingi wa Taarifa .......... 2
1.3 Mawanda ya Uchambuzi .......... 3
**SEHEMU YA PILI** .......... 4
**2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.** .......... 4
2.1 Ufafanuzi wa Jumla .......... 4
2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. .......... 5
2.2.1 Taarifa ya Fedha zilizovuka Mwaka 2024/2025 .......... 5
2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43 .......... 6
2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05 .......... 7
2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida .......... 9
2.2.5 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo .......... 15
2.2.6 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati .......... 18
**SEHEMU YA TATU** .......... 19
**3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** .......... 19
3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 .......... 19
3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida .......... 21
**SEHEMU YA NNE** .......... 26
**4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** .......... 26
4.1 Maoni ya Jumla .......... 26
4.2 Wizara ya Kilimo – Fungu 43 .......... 27
4.3 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05 .......... 31
4.4 Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24 .......... 32
**SEHEMU YA TANO** .......... 34
**5.0 HITIMISHO** .......... 34
5.1 Maelezo ya Kuhitimisha .......... 34

## ORODHA YA MAJENDWALI

**JEDWALI NA: 1** FUNGU 43 - MAKADIRIO NA MAKUSANYO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ....... 6

**JEDWALI NA: 2:** FUNGU 05 - MAKADIRIO NA MAKUSANYO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ...... 8

**JEDWALI NA: 3:** FUNGU 43 MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/2026 .................. 10

**JEDWALI NA: 4:** LIFUATALO LINAONYESHA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUPOKELEWA KWA KILA MRADI ........ 10

**JEDWALI NA: 5:** FUNGU 05 MAPOKEZI FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA ........ 13

**JEDWALI NA: 6:** FUNGU 15 MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/2026 .................. 15

**JEDWALI NA: 7:** ULINGANISHO KATIKA MAKUSANYO YA MADUHULI FUNGU 43 ........ 20

**JEDWALI NA: 8:** ULINGANISHO KATIKA MAKUSANYO YA MADUHULI FUNGU 05 ........ 21

**JEDWALI NA: 9:** MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 IKILINGANISHWA NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........ 22

**JEDWALI NA: 10:** MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 IKILINGANISHWA NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........ 24

**JEDWALI NA: 11:** MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 IKILINGANISHWA NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........ 25

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

---

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/ 2027.

**Mheshimiwa Spika**, **Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na
e) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(b) na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekekezaji na Makadiriro ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilifanya uchambuzi na kupata maudhui ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na uchambuzi na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge yanayohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Kazi hiyo ilifanyika kati ya tarehe 15 na 18 Machi 2026

katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo.

## 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inagusa mafungu matatu. **Fungu 43** ambalo ni Wizara ya Kilimo, **Fungu 24** - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na **Fungu 05** - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mafungu yote matatu tarehe 19 na 23 Machi 2026.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 19 na 23 ya Mwezi Machi, 2026. Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Wizara ya Kilimo zilizohusu pamoja na mambo mengine Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo iliwasilishwa na **Mhe. Daniel Godfrey Chongolo Mb**, Waziri wa Kilimo. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hizo umeangazia maeneo makuu manne yafuatayo;

a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya kawaida na Mendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari 2026;

c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** mambo hayo yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu, Wizara ya Kilimo - **Fungu 43**, Tume ya Maendeleo ya Ushirika - **Fungu 24** na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05**.

### 2.2.1 Taarifa ya Fedha zilizovuka Mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo (Fungu 43) iliomba kibali cha kuvuka na jumla ya **Shilingi 48,791,570,661** ili kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo zikiwemo kugharamia ununuzi wa mbolea, ruzuku za mbolea, ununuzi wa nafaka na kugharamia madeni yalitotokana na biashara ya Pamba msimu wa kilimo 2019/2020. Kampuni ya Mbolea Tanzania-TFC **Shilingi 15,000,000,000**, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania – TFRA **Shilingi 15,000,000,000,** Wakala wa Taifa wa Hifadhi za Chakula-NFRA **Shilingi 4,000,000,000** na Bodi ya Pamba Tanzania-TCB **Shilingi 14,791,570,661.** Hadi kufikia Februari 2026 fedha zote **Shilingi 48,791,570,661** zilipokelewa.

Aidha kwa upande wa **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji-Fungu 05** fedha zilizovuka mwaka 2024/2025 ni **Shilingi 23,035,020,861.95** ambapo fedha hizo zilitumika kulipa madai ya wakandarasi.

### 2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Kilimo Fungu 43 ililenga kukusanya maduhuli jumla ya **Shilingi 8,665,370,000** kutoka Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo yanatokana na Ukaguzi wa Mazao, Kodi za Mazao na Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni na **Shilingi 24,219,196,666.66** kutoka Mfuko wa Mendeleo ya Kilimo.

Hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 Wizara ya Kilimo ilikuwa imekusanya **12,962,023,810.69** sawa na **Asilimia 149.58** ya malengo yaliyokusudiwa kutoka kwenye Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 29,288,658,829.92** sawa na **Asilimia 120.93** kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na.01.**

**Jedwali Na: 1 Fungu 43 - Makadirio na Makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| **MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2025/2026** | | | |
|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio (tsh.)** | **Makusanyo (tsh.)** | **Asilimia** |
| Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali | 8,665,370,000 | 12,962,023,810.69 | 149.58 |
| Mapato ya Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo | 24,219,196,666.66 | 29,288,658,829.92 | 120.93 |
| **Jumla** | **32,884,566,666.66** | **42,250,682,640.61** | **128.48** |

**Chanzo:** Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 42,250,682,640.61** sawa na **Asilimia 128.48** ya makusanyo yote yalikusanywa katika kipindi hicho. Ukusanyaji huo wa mapato unaonyesha kuwa umevuka malengo ambayo Wizara ilijiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huu ni wazi kuwa Wizara inaweza kufanya tathmini na kuongeza lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa kuimarisha matumizi ya Mfumo wa e-kilimo katika ukusanyaji wa mapato na kuthibiti utoroshaji wa mazao Mipakani.

### 2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi 3,600,000,000**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Tume ya Umwagiliaji ilikuwa imekusanya **Shilingi 1,908,588,429.88** sawa na **asilimia 53.02** ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali namba 2.

**Jedwali Na: 2: Fungu 05 - Makadirio na Makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2025/2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio (tsh.)** | **Makusanyo (tsh.)** | **Asilimia** |
| Fungu 05 | 3,600,000,000 | 1,908,588,429.88 | 53.02 |

**Chanzo:** Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 05

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo ya maduhuli kwa fungu 05 yanaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa katika Fungu hili hadi kufikia Mwezi Februari 2026 ni Shilingi **1,908,588,429.88** sawa na **asilimia 53.02** ya lengo kwa mwaka. Kiwango hicho cha makusanyo si cha kuridhisha, kwani hadi Februari, 2026 kiwango cha makusanyo kilipaswa kufikia **asilimia 75.**

**Mheshimiwa Spika**, Kushindwa kukusanya maduhuli kwa kiwango kinachotosheleza cha asilimia, kuna punguza uwezo wa Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. **Ili kuondokana na athari hizo, ni rai ya Kamati kuwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iongeze kasi na kubuni mikakati itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kupitia mifumo mathubuti ili kufikia lengo lililokusudiwa katika mwaka wa fedha 2026/2027**.

### 2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka Fedha 2025/2026 Wizara ya Kilimo imeidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,192,975,075,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24.

#### 2.2.4.1 Fungu Na.43 Wizara ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 135,983,889,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 81,447,048,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara, Bodi na Taasis na **Shilingi 54,536,841,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara, Bodi na Taasisi. Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa **Shilingi 652,275,933,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 424,328,013,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 227,947,920,000** ni fedha za nje.

Hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 65,180,207,771.44** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 47.93** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hzio **Shilingi 14,549,642,218.88** matumizi mengineyo na **Shilingi 50,630,565,552.56** ni kwa ajili ya mishahara.

Kwa upande wa fedha za maendeleo hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 361,292,488,068.57** sawa na **Asilimia 55.39**. kati ya fedha hizo **Shilingi 197,639,844,258.98** sawa na **Asilimia 46.58** ni fedha za

ndani na **Shilingi 163,652,643,809.59** sawa na **Asilimia 71.79** ni fedha za nje. Jedwali namba 3 linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 43 kwa Mwaka 2025/2026.

**Jedwali Na. 1 -**

**Jedwali Na: 3: Fungu 43 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2025/2026**

| MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/202 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | | **Fedha iliyotengwa 2025/2026** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | | **81,447,048,000.00** | **50,630,565,552.56** | 62.16 |
| Oc | | **54,536,841,000.00** | **14,549,642,218.88** | 26.68 |
| **Jumlandogo(matumizi ya kawaida** | | **135,983,889,000.00** | **14,763,572,470.05** | **47.93** |
| **Maendeleo** | **Ndani** | **424,328,013,000** | **197,639,844,258.98** | **71.79** |
| | **Nje** | **227,947,920,000** | **361,292,488,068.57** | **55.39** |
| **Jumla Kuu** | | **788,259,822,000** | **426,472,695,840.01** | **54.10** |

**Chanzo***:* Randama ya Wizara Fungu 43

**Jedwali Na: 4: Iifuatalo linaonyesha miradi ya maendeleo iliyotengewa Fedha na kupokelewa kwa kila mradi**

| MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2025/2026 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Bajeti iliyotengwa 2024/2025** | | **Mapokezi ya fedha hadi kufikia Februari 2026** | | **Asilimia ya mapokezi** | |
| | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** | **fedha za ndani** | **fedha za nje** | **Ndani** | **Nje** |
| 4429: Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi(AFDP) | | 31,246,503,540 | 0 | 8,334,783,893 | | 26.67 |
| 4430: Mradi wa kuwezesha upatikaji wa pembejeo za Kilimo Tanzania (TAISP) | 221,800,000,000, | 40,000,000,000 | 61,000,000,000 | 6,506,899,505 | 27.50 | 16.27 |
| 4431 Mradi wa Jenga kesho iliyo Bora (BBT) | 16,000,000,000 | 41,009,000,000 | 6,000,000,000 | 14,502,899,505 | 37.50 | 35.36 |
| 4403 Program ya Mifuko himilivu ya Chakula Tanzania (TFSRP) | 185,071,116,400 | 130,736,000,000 | 129,882,960,658 | 128,232,558,184 | 70.18 | 98.09 |
| 4497 Mradi wa kuongeza uwezo wa uhifadhi | 700,000,000 | 28,880,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4499 Mradi wa kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC) | 756,883,600 | 6,076,396,460 | 756,883,600 | 6.076,396,459 | 100 | 100 |
| **Jumla Kuu** | **424,328,000,000** | **277.947,900,000** | **197,639,844,259** | **163,652,643,810** | **46.58** | **58.88** |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 43*

**Mheshimiwa Spika**, tamthimi ya mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida si wa kuridhisha kwani ni **asilimia 47.93** ya fedha iliyotengwa imepokelewa. Endapo hali hiyo itaendelea kuwa si kuridhisha hadi itakapofika mwezi Juni 2026 wakati wa kuhitimisha mwaka huu wa fedha, ni Dhahiri kuwa Wizara itashindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo;

(a) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa Miradi ya Maendeleo ni **Asilimia 55.39** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo.

(b) Mradi wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) uliidhinishiwa jumla ya Shilingi **16,000,000,000** fedha za ndani**,** hadi kufikia Februari, 2026 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 37.50** ya Bajeti. Utolewaji huu wa fedha umeathiri utekelezaji wa miradi ya BBT na hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo ya kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye Kilimo.

(c) Mtiririko huu wa fedha kwenye miradi ya maendeleo unaathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa kwenye mradi wa Upatikananaji wa Pembejeo za Kilimo Tanzania, Program ya Maendeleo ya Kilimo, ambayo

tayari ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji wake. Jambo linaloathiri utekelezaji Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kilichoahidi kuendelea kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinaendelea kuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa.

#### 2.2.4.2 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu – 05** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 73,416,447,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,267,617,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 65,148,830,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha Fedha za Maendeleo ni **Shilingi 308,721,961,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 259,617,801,000** fedha za ndani na **Shilingi 49,104,160,00**0 ni fedha za nje.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, fedha za matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni **Shilingi 9,415,070,368.75** sawa na **asilimia 14** ya fedha iliyoidhinishwa na Fedha za Maendeleo kiasi cha **Shilingi 141,259,519,828.31** sawa na **asilimia 45.7.** Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 5**.

### Jedwali Na: 5: Fungu 05 Mapokezi Fedha za Matumizi ya Kawaida

| MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | | **Fedha iliyotengwa 2025/2026** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | | 8,267,617,000 | 5,784,281,500 | 69.96 |
| Oc | | 65,148,830,000 | 3,430,788,869 | 5.2 |
| **Jumlandogo(matumizi ya kawaida** | | **73,416,447,000** | **9,415,070,368.75** | **14.45** |
| **Maendeleo** | **Ndani** | **259,617,801,000** | **102,082,179,525.32** | **39.32** |
| | **Nje** | **49.104,160,000** | **39,187,340,303** | **79.80** |
| **Jumla Kuu** | | **382,138,408,000** | **150,684,590,192** | **39.43** |

**Chanzo***:* Randama ya Wizara Fungu 05

**Mheshimiwa Spika**, tathmini inaonesha kuwa, hadi februari, 2026, upatikanaji wa fedha za bajeti katika Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo hauridhishi. Uchambuzi zaidi wa Kamati unaonesha kuwa, kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo zililenga kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha kutolewa kwa fedha za Matumizi ya kawaida kwa **asilimia 14.45** tu kwa kiasi kikubwa kunakwamisha uendeshaji wa majukumu ya Tume.

**Mheshimiwa Spika**, kutokupokelewa kwa fedha za miradi iliyotengwa kikamilifu, kuna athari kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ya kushindwa kutekeleza azma yake ya kuongeza uzalishaji wa chakula na usimamizi wa mipango iliyokusudiwa kutekelezwa. **Ni maoni ya Kamati kuwa, fedha za maendeleo hususan fedha zilizotengwa kutekeleza miradi**

**ya sekta ya umwagilaji zitolewe ili kukamilisha miradi iliyokusudiwa kutekelezwa na kupunguza malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na wazabuni jambo linalopelekea kuongezeka kwa madeni kutokana na riba na hivyo kupelekea hasara kwa serikali.**

### 2.2.4.3 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika - **Fungu – 24** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 21,879,669,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 12,846,074,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 9,033,595,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha Fedha za Maendeleo ni **Shilingi 697,176,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 418,305,600** fedha kwa ajili ya kuimarisha ushirika wa Bustani za mazao mbogamboga(TCDC) na **Shilingi 49,104,160,00**0 ni fedha za ukarabati wa Ofisi za COASCO.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, fedha za matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni **Shilingi 9,415,070,368.75** sawa na **asilimia 58.30**ya fedha iliyoidhinishwa na Fedha za Maendeleo kiasi cha **Shilingi 278,880,000 (COASCO)** sawa na **asilimia 40** kilipokelewa**.** Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na: 6: Fungu 15 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2025/2026**

| MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2025/2026** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | 12,846,074,000 | 10,472,835,670 | 81.52 |
| Oc | 9,033,595,000 | 2,284,053,472.26 | 47.44 |
| Maendeleo | 697,176,000 | 278,870,400 | 40 |
| Jumla | 22,576,845,000 | 13,035,759,542 | 57.73 |

**Chanzo:** *Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 24*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha kwa Fungu 24- Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaonekana kuwa si ya kuridhisha kwa upande wa fedha za maendeleo. Endapo hali hiyo itaendelea kuwa si ya kuridhisha hadi itakapofika mwezi Juni, 2026 wakati wa kuhitimisha mwaka wa fedha wa 2025/2026, ni dhahiri kuwa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu haitatekelezwa mathalani mradi wa kuimarisha ushirika wa Bustani za mazao mbogamboga(TCDC) ambao ulitengenewa **Shilingi 418,305,600** na hakuna fedha iliyopokelewa. **Kamati inashauri kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe ipasavyo ili wananchi waweze kunufaika na miradi iliyopangwa kutekelezwa**.

### 2.2.5 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara ya Kilimo na Mafungu yake matatu. Kamati ilitembelea na kukagua miradi miwili iliyopo Morogoro na Dodoma kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya

120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

i. **Mradi Namba 6260** – **Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Taifa ya Mbegu TOSCI – Morogoro.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Taifa ya Mbegu TOSCI-Morogoro. Ukarabati huo ulilenga kuongeza ukubwa kutoka Mita za Mraba 825 na kufikia Mita za Mraba 1,715 jambo linaloongeza Maabara Mahsusi kutoka tatu na kufikia 4, Ofisi za Wataalam 7 na kufikia 19. Mradi huu ulianza tarehe 19 Septemba 2024 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 17 Machi 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa mradi huu hadi kukamilika unatarajiwa kugharimu jumla ya **Shilingi 1,988,144,792.79** ikiwa ni fedha za ufadhili kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo. Hadi kufikia tarehe 2 Machi 2026 jumla ya **Shilingi 1,224,059,637.51** zimetumika kwa shughuli za utekelezaji wa mradi saw ana asilimia 61.6 ya bajeti ya mradi. Aidha utekelezaji wa mradi umeikia **asilimia 86.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ililidhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi huu na inaona kuwa kukamilika kwa mradi huu utaongeza uwezo wa kudhibiti ubora wa mbegu kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendelea kulinda taswira ya Tanzania katika viwango vya ubora wa

mbegu kimatifa na kufunga fursa mpya kwa uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbegu.

ii. **Mradi Na. 4486 – Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagilijaji katika Kituo cha TARI- Hombolo Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa TARI kupitia kituo cha TARI Hombolo inatekeleza mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji wenye ukumbwa wa hekta 70. Mradi huu ni sehemu ya mradi wa umwagiliaji wa vituo 11 vya TARI na unatarajia kugharimu 17,818,629,997.28. Mradi huu ulianza kutekelezwa Mwezi Mei 2024 na unatarajia kukamilika Mwezi Juni 2026, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa ujenzi wa Miundombinu ya kutoa maji katika Bwawa la Hombolo na kusafirisha mpaka mashambani ambako kunajengwa na kusimikwa miundombinu ya umwagiliaji aina ya *Centre Pivot* na *Gun Springler system***.** Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha kazi za utafiti wa kilimo na kuwezesha majaribio kufanyika kwa mwaka mzima,kuongeza eneo la uzalishaji mbegu kutoka hekta 3.6 hadi 73.6, kuongeza mapato ya ndani yanayotokana na mauzo ya mbegu kutokana na ongezeko la uzalishaji wa mbegu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza **Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuwekeza kwenye miundombinu ya umwagiliaji na utafiti itakayosaidia Wizara kupitia Taasisi zake kugundua, kubuni na kuongeza upatikanaji wa teknolojia zinazojibu changamoto za Kilimo Nchini. Teknologia hizi zitawafanya Wakulima kuongeza tija katika uzalishaji na hivyo kuchangia kuondoa umaskini na kukuza uchuni wa mtu mmojammoj na Taifa kwa Ujumla**

### 2.2.6 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Licha ya utekelezaji huo mzuri, upatikanaji wa fedha usioridhisha umeendelea kuwa kikwazo kwa Wizara na hivyo kushindwa kuzingatia ipasavyo baadhi ya ushauri wa Kamati, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa maagizo yenye muendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, mnamo tarehe 23 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ta Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi. Tathmini ya uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**,katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Kilimo - Fungu 43 inaomba kuidhinishiwa kukusanya mapato jumla ya **Shilingi 61,000,000,000**. Kati ya fedha hizo Shilingi 25,000,000,000 maduhuli kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Shilingi 36.000.000.000 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo. Fedha inayotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la **asilimia 85** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa fungu unaonekana katika **Jedwali Na.7.**

**Jedwali Na: 7: Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli Fungu 43**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio Mwaka 2025/2026** | **Makadirio Mwaka 2026/2027** | **PUNGUFU/ ONGEZEKO** | **Asilimia** |
| Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali | 8,665,370,000 | 25,000,000,000 | 16,334,630,000 | 188.72 |
| Mapato ya Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo | 24,219,196,666.66 | 36,000,0000,000 | | 35.82 |
| **Jumla** | **32,884,566,666.66** | **42,250,682,640.61** | **11,780,803,334** | **85** |

**Chanzo:** Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, Tathmini inaonyesha kuwa makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 85** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo uzoefu wa ukusanyaji kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ulionesha kumudu kukusanya **asilimia 128.48** hadi kipindi cha robo tatu ya kipindi cha utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kufikia **asilimia 85** ndani ya robo tatu ya Mwaka. Kamati ina amini kuwa upo uwezekano wa kufikia na kuvuka lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 endapo Wizara itaimarisha ukusanyaji wa tozo za mazao na kuthibiti utoroshaji wa mazao sehemu za mipakani jambo linalopelekea upotevu wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 05 -** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 3,600,000,000** ambayo ni sawa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha

2025/2026. **Jedwali Na. 6** linaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

**Jedwali Na: 8: Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli Fungu 05**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio 2025/2026 (tsh.)** | **Makadirio 2025/2026 (tsh.)** | **Ongezeko/ Pungufu** | **Asilimia** |
| Mfuko wa NIDF | 3,600,000,000 | 3,6,000,000,000 | 0 | 0 |

**Chanzo:** Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 05

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba, kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2026/2027 ni sawa na lengo la maduhuli ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati inaishauri Tume kuweka mikakati thabiti itakayowezesha kuongeza makusanyo ya mapato ikiwa ni pamoja kutumia Mifumo.

## 3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka Fedha 2026/2027 Wizara ya Kilimo inaomba kuidhinishiwa jumla ya **1,106,064,979,995** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24. Ikiwa ni punguzo la **asilimia 7**.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, inaomba kuidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 131,639,854,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya

fedha hizo **Shilingi 84,956,697,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara, Bodi na Taasis na **Shilingi 46,683,157,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara, Bodi na Taasisi. Kiasi hicho ni punguzo ya **asilimia 3.19** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 567,345,730,000**. Kiasi hicho ni punguzo la **asilimia 13** Mchanganuo kama unavyoonyesha kwenye jedwali Na.7

**Jedwali Na: 9: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | | **Makadirio 2025/2026** | **Makadirio 2026/2027** | **Ongezeko/ punguzo** | **Asilimi** |
| Mishahara | | **81,447,048,000.00** | **84,956,697,000** | 3,509,649,000 | 4.30 |
| Oc | | **54,536,841,000.00** | **46,683,157,000** | -7,853,684,000 | 14.40 |
| **Jumlandogo(matumizi ya kawaida** | | **135,983,889,000.00** | **131,639,854,000** | **-4,344,035,000** | **-3.19** |
| **Maendeleo** | **Ndani** | **424,328,013,000** | **360,678,811,000** | **-63,649,202,000** | **-15** |
| | **Nje** | **227,947,920,000** | **206,666,919,000** | **-21,281,001,000** | **-9.33** |
| **Jumla Kuu** | | **788,259,822,000** | **698,985,575,000** | **-89,274,247,000** | **-11.32** |

**Chanzo***:* Randama ya Wizara Fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Mwaka 2026/2027 ya Wizara ya Kilimo kwa mafungu yote matatu imepungua kwa kiasi cha **Shilingi 86,910,095,005** sawa na punguzo la **asilimia 7** ikilinganishwa na bajeti ya 2025/2026. Uchambuzi umebaini kuwa punguzo hilo linatokana pia kupungua kwa fedha za

matumizi ya kawaida kwa Fungu 43- Wizara ya Kilimo ambapo imepungua kwa **asilimia 11.32,**

**Mheshimiwa Spika,** Ufanisi wa utakelezaji wa miradi ya maendeleo hususani usambazaji wa mbolea pamoja na pembejeo za kilimo, unategemea upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ipo haja ya kuongeza bajeti ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya sekta hii na kuhakikisha tija inaongezeka katika kilimo. Kuongezeka kwa bajeti kutaboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Upande ya **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05.** Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 **Tume**, inaomba kuidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 75,568,800,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,419,970,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 65,148,830,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi hicho ni ongezeko la **a silimia 5.63** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 308,721,961000**. Hakuna ongezeko lolote kwenye fedha za

maendeleo. Mchanganuo kama unavyoonyesha kweny jedwali Na.10

**Jedwali Na: 10: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | | **Makadirio 2025/2026** | **Makadirio 2026/2027** | **Ongezeko /Pungufu** | **%** |
| Mishahara | | 8,267,617,000 | **10,419,970,000** | 2,152,353,000 | 26.03 |
| Oc | | 65,148,830,000 | **65,148,830,000** | 0 | 0 |
| **Jumlandogo(matumizi ya kawaida** | | **73,416,447,000** | **75,568,800,000** | **2,152,353,000** | **2.93** |
| **Maendeleo** | **Ndani** | **259,617,801,000** | **259,617,801,000** | **0** | **0** |
| | **Nje** | **49.104,160,000** | **49,104,160,000** | **0** | **0** |
| **Jumla Kuu** | | **382,138,408,000** | **384,290,761,000** | **2,152,353,000** | **5.63** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara Fungu 05

**Mheshimiwa Spika,Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika Fungu 24.** Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 inaomba kuidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 21,976,594,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 13,846,358,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 8,130,236,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi hicho ni punguzo la **asilimia 0.42** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026**.**

Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 697,176,000**. Mchanganuo kama unavyoonyesha kweny jedwali Na.9

**Jedwali Na: 11: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Makadirio 2025/2026** | **Makadirio 2025/2026** | **Ongezeko/ Punguzo** | **%** |
| Mishahara | 12,846,074,000 | 13,846,358,000 | 1,000,284,000 | 7.78 |
| Oc | 9,033,595,000 | 8,130,236,000 | -903,359,000 | 9.99 |
| Maendeleo | 697,176,000 | 697,176,000 | | 40 |
| Jumla | 22,576,845,000 | 13,035,759,542 | | 57.73 |

***Chanzo:*** *Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 24*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imepungua ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026 ,Aidha fedha kwaajili ya Miradi ya Maendeleo haijaongezeka. Punguzo la bajeti inaweza kuathiri kufikia malengo yaliyowekwa katika mpango wa kuendelea kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo. Kamati inaishauri serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Tume hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia majadiliano ya kina yaliyofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote yaliyo Wizara ya Kilimo kama ifuatavyo:

(i) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua, Kutokana na hali hiyo miradi mbalimbali imeathirika kutokana na kuongezeka kwa madeni ya wazabuni wanaosambaza mbolea kwa mpango wa ruzuku, wakandarasi wa miradi ya umwagiliaji, kupungua kwa ufanisi wa ufanyaji wa tafiti za kilimo pamoja na uzalishaji wa mbegu. Kamati inaishauri Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio ikiwa ni pamoja na kulipa madeni ya Makampuni yanayouza mbegu za mahindi kupitia program ya Ruzuku ya mbegu kiasi cha **Shilingi 54,917,779.249**. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya

mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za nje umekuwa wa kusuasua.

## 4.2 Wizara ya Kilimo – Fungu 43

(a) Kupungua kwa fedha iliyotengwa kwenye Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa **asilimia 7** kunakinzana na makubaliano ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014) yanayozitaka nchi wanachama kutenga **asilimia 10** ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo. Kamati inaendelea kushauri kwamba Serikali iendelee kuongeza bajeti ya kilimo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kutekeleza makubaliano ya maazimia ambayo nchi yetu imeingia

(b) Makusanyo hafifu ya maduhuli kutoka kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato ya Wizara hii yanatokana na changamoto ya udhibiti usiotosheleza wa maeneo ya mipaka ambapo unapelekea baadhi ya mazao kutoka nje ya nchi bila kukaguliwa katika vituo vya mipakani hivyo kupelekea kupoteza mapato ya Serikali. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha inashirikiana na mamlaka nyingine za Serikali katika utozaji wa tozo za mazao ili kuimarisha maduhuli ya Serikali na vilevile iongeze wakaguzi wa mazao katika vituo vya mipakani.

(c) Kusimama kwa mchakato wa kutunga Sheria ya Kitaifa Kusimamia Rasilimali za Nasaba za Mimea kwa takribani miaka 18 kumepelekea Wakulima kutokuwa na Sheria inayolinda Mbegu za Asili na Haki za Wakulima. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa utungaji wa Sheria hii ili mbegu za asili ziweze kutambulika na kulinda haki za mkulima wa mbegu. Aidha kuwepo kwa sheria kutasaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu za asili na hivyo kusaidia upatikanaji wa lishe bora na kuchangia kujitosheleza kwa virutubisho na kupunguza ulazima wa uhitaji wa virutubisho vya viwandani.

(d) Kutokana na athari zinazoweza kujitokeza kwenye Tasnia ya Mbolea nchini kufuatia migogoro inayoendelea kati ya Marekani/ Israeli na Irani jambo ambalo litapelekea kupanda kwa bei ya mbolea pamoja na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi na hivyo kupelekea kupanda kwa gharama za uzalishaji kwa wakulima nchini. Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo

(i) Kuviwezesha viwanda vinavyozalisha mbolea na visaidizi vya mbolea ndani ya nchi kwa kutekeleza mpango Maalumu wa Ruzuku ili kupunguza gharama za uzalishaji.

(ii) Kuwa na Mpango Mahsusi wa kuhakikisha mbolea inapatikana kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwezesha Kampuni zinazoagiza mbolea nchini kuingiza mbolea

kutoka maeneo mengine yanayozalisha mbolea Duniani.

(iii) Kulipa madai ya Makampuni yanayouza mbolea kupitia programu ya Ruzuku ya Mbolea kiasi cha **Shilingi 398,320,133,180,** kati ya kiasi hicho TFC inadai takribani **Shilingi 43,022,740,822.**

(e) Kutokana na kufungwa kwa Viwanda Vingi vya Chai Nchini, soko la zao la Chai limekuwa changamoto kubwa jambo linalopelekea kuinyima sekta ya kilimo fursa ya kuchangia ipasavyo katika uchumi ikiwa ni pamoja na kuwakatisha tamaa wakulima. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi ikiwa ni pamoja na kutafuta Wawekezaji wenye uwezo wa kuendesha Viwanda vya Chai Nchini na kutafuta masoko ya nje ya nchi. Aidha Serikali iandae mkakati mahsusi wa kuinuna zao la Chai nchini kwa kutatua changamoto mbalimbali ili Wananchi waendelee kulima zao la chai. Vilevile Serikali iweke Mkakati wa kuwawezesha Wakulima kuwa na Viwanda vidogovidogo vya kusindika Chai.

(f) Matumizi ya Zana za Kisasa za Kilimo bado ni changamoto kwa Wakulima wengi Nchini, asilimia 44 ya Wakulima bado wanatumia jembe la mkono jambo linalopelekea wakulima wengi kuzalisha bila tija. Kamati inaishauri Serikali kuongeza upatikanaji wa Huduma za Zana za Kisasa kwa kununua Matrekta na *Powertille*r pamoja na zana nyingine na vilevile

kuongeza Vituo vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo ili kuongeza upatikanaji wa huduma za zana za kisasa kwa wakulima na, kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija. Aidha Kamati inaishauri Serikali iandae Mwongozo Maalum wa usimamizi na uendeshaji wa Vituo hivyo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa Zana hizi hukosa usimamizi na kuharibika. Aidha Serikali ihakikishe inatafuta wawekezaji wa Viwanda vya Zana za Kilimo Nchini ili kupunguza bei za zana hizo na kuongeza upatikanaji.

(g) Matumizi yasiyosahihi ya pembejeo za kilimo yaani mbegu bora, viuatilifu na mbolea vinapelekea wakulima wengi kupunguza uzalishaji, uharibifu wa udogo, ubora mdogo wa mazao. Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ili kufikia lengo la kuongeza uzalishaji na ukuaji wa kilimo na kufikia asilimia 10 ifikapo 2030 na vilevile kupunguza athari za viuatilifu kwa binadamu. Aidha Serikali iendelee kuboresha huduma za Ugani kwa kuwapatia vitendea kazi.

(h) Kutotolewa kwa fedha za mradi wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) ambapo kiasi cha fedha kilichopokelewa ni **Shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 37.50** ya fedha za ndani zilizotengwa jambo ambalo limeathiri utekelezaji wa miradi ya BBT. Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi cha fedha kilichobaki kabla Mwaka huu wa fedha kuisha ili kufanikisha utekelezaji wa mradi kutokana na umuhimu wa mradi huu

katika kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake na hatimaye kufikia lengo la kutengeneza ajira 3,000,000 za vijana na wanawake ifikapo 2030.

(i) Maendeleo ya Sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kuhusu sekta husika. Sekta ya kilimo inakumbwa na changamoto ya watafiti kuondoka na kwenda kufanya kazi ambazo siyo za kitafiti jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa shughuli za kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa watafiti ikiwemo kuboresha maslahi ya watafiti, mazingira ya kazi pamoja na kupata Hatimiliki za Ugunduzi.

## 4.3 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

(a) Kutotolewa kwa fedha za miradi ya sekta ya umwagiliaji kumepelekea kuchelewa kwa malipo ya Wakandarasi, Washauri elekezi jambo ambalo limeathiri utekelezaji wa miradi ya sekta ya umwagiliaji. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na Miradi **51** iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2025/26 kutoanza utekelezaji wake hadi tarehe 25 Machi, 2026 wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umwagiliaji wanadai jumla ya **shilingi 109,189,941,826.84 na** Miradi **101** iliyokuwa ikitekelezwa kabla ya mwaka 2025/2026 kusimama, jambo ambalo litaisababishia Serikali hasara kwa sababu mvua zinazoendelea nchini zinaweza kuathiri miradi hiyo na hivyo Serikali kuingia gharama mara mbili. Kamati inaishauri Serikali kulipa hati zote za madai ambazo zimewasilishwa Wizara ya Fedha zenye jumla ya **shilingi 109,189,941,826.84.** Aidha,

Kamati inaishauri Serikali kukwamua miradi yote iliyokwama ili kudhibiti hasara inayoweza kujitokeza.

(b) Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti katika miradi ya sekta ya umwagiliaji ili kuweza kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye Mabonde, Umwagiliaji mdogo mdogo wa kutumia maji ya maziwa, visima na mito isiyokauka ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile Ngano, Mchele, Miwa yatakayoweza kutosheleza mahitaji ya ndani ya nchi na nje ya nchi, na hivyo kuongeza thamani ya mauzo ya nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Billioni 1.2 hadi Dola za Marekeni Bilioni 5 ifikapo 2030. Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha maalumu kwa ajili ya miradi mikubwa ya umwagiliaji ya Kimkakati katika mabonde makubwa kama Kilombelo na Ruvu.

## 4.4 Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24

(a) Kutotolewa kwa fedha za Mradi wa Kuimarisha Ushirika wa Bustani za Mazao ya Mbogamboga (TCDC) kiasi cha **Shilingi 428,305,600.00** kumesababisha mradi huu kutotekelezwa kabisa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani.

(b) Kukosekana kwa Mpango Madhubuti wa ufufuaji wa Viwanda vya Vyama vya Ushirika kunapelekea kukosekana kwa ushindani wa masoko nchini hasa katika zao la pamba, Kahawa, tumbaku na mazoa mengine. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha vyama vya ushirika kwa

kuhakikisha mipango ya uwekezaji ikiwa pamoja na kufufua Viwanda vya Vyama vya Ushirika inatekelezwa ili vyama hivyo vijiendeshe kibiashara na kiushidani.

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

## 5.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa;

1. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, - Mjumbe
5. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Tauhida Galos Cassian, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - Mjumbe

9. Mhe. Omar Marcus Msigwa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobelo, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Dkt.Rita Enerpher Kabati, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde Mb - Mjumbe
14. Mhe. Magreth Baraka Ezekiel, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Abubakar Alli Omari, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Khalfan Issa Mohamed, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi - Mjumbe
19. Mhe. Khamis Hamad Yussuf, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amour Seif Abdalla, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khalid Mussa Nsekela, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo kwa kipindi chote cha uongozi wake, Mhe. Daniel Godfrey Chongolo (Mb) - Waziri wa Kilimo na Mhe.

David Ernest Silinde (Mb) – Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Makatibu Prof. Peter Msoffe na Ndg. Athumani Kilundumya

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuwangoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43, 24 na 05), kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Deodatus Philip Mwanyika (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

April, 2026